







# Mkataba wa Minamata Kuhusu Zebaki

MINAMATA CONVENTION ON MERCURY

## Ofisi ya Makamu wa Rais

# Yaliyomo


1. Sifa, Matumizi na Madhara ya Zebaki
2. Mchakato, Nembo na Vipengele Muhimu vya Mkataba
3. Uridhiaji wa Mkataba
4. Dondoo za Mpango-kazi wa Taifa
5. Hitimisho

# Zebaki

- Zebaki halisi *(pure)* iko katika hali ya kimiminika kizito.



- Uchafuzi wa Zebaki huchangiwa na matukio ya asili na shughuli za binadamu.

- Zebaki ni moja ya vyanzo kumi (10) vinavyohatarisha zaidi afya ya jamii duniani *(Shirika la Afya Duniani – WHO)*



# Sifa za Zebaki

- Husafiri masafa marefu
- Hudumu kwa muda mrefu
- Hujilimbikiza katika mfumo mfuatano wa chakula
- Madhara kwa afya na mazingira.



# Matumizi ya Zebaki

## Afya



## Viwanda




## Madini



## Utafiti





# Madhara ya Kiafya ya Zebaki

- Huathiri mfumo wa neva za fahamu
  - Kusikia, kuongea, kuona, kumeng'enya na kumeza chakula
  - Kutembea na ukakamavu wa mwili

- Huathiri viungo muhimu vya mwili – moyo, mapafu, ini, figo na hata mimba.



# Mchakato wa Kuandaa Mkataba

| | |
|---|---|
| UNEP ilielekezwa kufanya tathmini | 2001 |
| Tathmini ya Kwanza | 2002 |
| Hatua za hiyari | 2003 |
| Azimio la kuanzisha Mkataba | 2009 |
| Vikao 5 vya majadiliano | 2010-2013 |
| Kusainiwa Mkataba | 2013 |
| Kuanza kutekelezwa | 2017 |

# Nembo ya Mkataba

- Umbo la Samaki anayeogelea – hamasa na mshikamano.
- Rangi nyeusi - madhara ya Zebaki na hatari inayoikabili Dunia.
- Rangi ya dhahabu – maono na matarajio ya mafanikio *(golden future)*



# Nchi Zilizoridhia Mkataba

Nchi Zilizoridhia Mkataba = **113** (31 Agosti, 2019)



# Nchi Zilizoridhia Mkataba (2)

- Tanzania ilitia saini tarehe 10 Oktoba, 2013





**Mhe. Terezya Huvisa**
*10 Oktoba, 2013*
*Japan*




# Vipengele Muhimu vya Mkataba

# Mkataba wa Minamata

- Mkataba una jumla ya Ibara 35 (na Viambatisho 4) :
  - i) Majukumu ya nchi wanachama
  - ii) Ufadhili kwa nchi wanachama
  - iii) Taarifa na kukuza uelewa
  - iv) Masuala ya kiutawala



# Ibara ya 1: Madhumuni

- Kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yanayotokana na uchafuzi wa mazingira unaotokana na Zebaki




- Vyanzo vya uchafuzi ambapo Zebaki inatumiwa kwa kudhamiria au kujitokeza kwa kutodhamiria.

# Ibara ya 3: Vyanzo na Biashara ya Zebaki

- Kupiga marufuku migodi mipya ya uchimbaji wa Zebaki baada ya Mkataba kuanza utekelezaji wake.
- Migodi iliyopo imepewa kipindi cha mpito cha miaka 15 baada ya Mkataba kuanza utekelezaji wake.
- Biashara inaruhusiwa baina ya Nchi Wanachama na zisizo Wanachama.

# Ibara ya 4: Bidhaa Zenye Viambata vya Zebaki

- Kusitisha uzalishaji, uingizaji na usafirishaji nje ya nchi wa bidhaa zenye viambata vya Zebaki ifikapo mwaka 2020.

- Kupunguza matumizi ya Zebaki katika tiba ya meno.












# Ibara ya 5: Shughuli za Uzalishaji Viwandani

- Kuzuia matumizi ya Zebaki katika shughuli za uzalishaji viwandani
- Kudhibiti uchafuzi wa mazingira endapo kuna kiwanda kinachotumia Zebaki
- Kubainisha viwanda vinavyotumia Zebaki

2002




2008




2013




2018



# Ibara ya 6: Maombi ya msamaha

- Kuomba msamaha wa kuendelea kutumia *bidhaa zenye viambata vya Zebaki* baada ya kipindi cha mpito mwaka 2020.

- Msamaha huu utakuwa ni wa miaka mitano (5) kuanzia tarehe ya kujiunga na nyongeza ya miaka mitano kwa kutegemea ridhaa ya Nchi Wanachama na haitazidi miaka kumi hadi kufikia 2030.

# Ibara ya 7: Uchimbaji Mdogo wa Madini ya Dhahabu

- Kupunguza, *na pale inapowezekana*, kuondosha matumizi ya Zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu.



- Hakuna ukomo wa matumizi ya Zebaki

- Kuandaa na kutekeleza Mpango-Kazi wa Taifa

# Ibara ya 8: Uchafuzi wa Hewa

- Kudhibiti vyanzo vya uchafuzi wa hewa:
  - mitambo ya viwandani inayotumia makaa ya mawe;
  - uzalishaji wa madini ya risasi, zinki, shaba na dhahabu;
  - mitambo ya uteketezaji wa taka;
  - viwanda vya saruji.

- Kubainisha vyanzo vya uchafuzi wa hewa unaosababishwa na Zebaki



# Ibara ya 9: Uchafuzi wa ardhi na maji

- Kubainisha vyanzo vya uchafuzi wa ardhi na maji unaosababishwa na Zebaki.

- Kuandaa Mpango wa Taifa unaolenga kupunguza au kuondosha uchafuzi.



# Ibara ya 11: Taka za Zebaki

- Kuhakikisha taka za Zebaki zinasimamiwa kikamilifu kwa kuzingatia miongozo chini ya Mkataba wa Basel unaodhibiti usafirishaji na utupaji wa taka hatarishi baina ya Nchi.

# Ibara ya 12: Maeneo Yaliyochafuliwa na Zebaki

- Kuandaa mkakati wa kubainisha na kutathmini maeneo yaliyochafuliwa na Zebaki

- Kuchukua hatua kupunguza uwezekano wa maeneo haya kuathiri afya ya jamii



# Ibara ya 13: Vyanzo na Utaratibu wa Upatikanaji wa Rasilimali Fedha

- Ibara hii imeainisha vyanzo na utaratibu wa upatikanaji wa rasilimali fedha za kutekeleza Mkataba ikiwa ni pamoja na:
  - Kutenga bajeti ya Serikali;
  - Mfuko wa Dunia wa Mazingira;
  - Washirika wa maendeleo; na
  - Sekta binafsi.

# Ibara ya 14: Kujenga Uwezo, Misaada ya Kitaalam na Uhawilishaji wa Teknolojia.

- Ibara hii inahimiza ushirikiano miongoni mwa Nchi Wanachama katika kujenga uwezo, kutoa misaada ya kitalaam na uhawilishaji wa teknolojia katika kutekeleza matakwa ya Mkataba.

# Ibara ya 16: Masuala ya Afya ya Jamii

- Kuandaa na kutekeleza mikakati na programu za kulinda afya ya jamii dhidi ya madhara ya Zebaki:
  - Kuboresha huduma za afya
  - Kujenga uwezo wa taasisi na wataalam wa afya



# Ibara ya 20: Mpango wa Utekelezaji wa Mkataba

- Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mkataba
- Ushirikishwaji wa wadau

# Mpango-Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu (2019-2024)








# Sekta ya Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu



10-20%

Milioni 1.2



20-30% Wanawake



Tani 13.2-24.4 za Zebaki




Mikoa 13 kati ya 26




25-33% ya Wachimbaji

# Dondoo za Mpango-Kazi wa Taifa

Miaka 5 (2019-2024)

Dola Milioni 10.7

Wadau 32

## Malengo

- Kupunguza matumizi ya Zebaki
- Kuimarisha mfumo wa sheria na uwezo wa kitaasisi
- Mkakati mahsusi wa kulinda afya ya jamii

## Shughuli za Kipaumbele

(29)

- Mbinu na teknolojia bora
- Mikopo nafuu
- Huduma za afya
- Kuwezesha wanawake na vijana
- Takwimu za kijiolojia
- Kanuni za Usimamizi wa Zebaki

# Hitimisho

MINAMATA
CONVENTION
ON MERCURY

MAKE
MERCURY
HISTORY